

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KILIMO



Anuani yaSimu: "Kilimo Dodoma"  
Nambari: +255 26 2321407  
Fax: +255 26 2320037  
**Email:** ps@kilimo.go.tz

Idara ya Utawala,  
Kilimo IV Dodoma,  
S.L.P. 2182,  
**DODOMA,**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MAADHIMISHO YA SIKU YA  
CHAKULA DUNIANI**

Dodoma, 01 Oktoba, 2020

Wizara ya Kilimo inapenda kuwataarifu wananchi na wadau wote wa sekta ya kilimo nchini kuwa **Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yatafanyika kitaifa mkoani Njombe kuanzia tarehe 10 Oktoba 2020 na kilele chake itakuwa tarehe 16 Oktoba 2020.**

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa leo (01.10.2020) na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Omari T. Mgumba(Mb.) jijini Dodoma imesema maandalizi ya maadhimisho hayo yamekamilika na kuwa wizara, taasisi, wakala, mashirika ya kimataifa na kitaifa zinakaribishwa kujitokeza kushiriki kwenye maadhimisho ya mwaka huu.

Kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani mwaka huu inasema "**Kesho Njema Inajengwa na Lishe Bora Endelevu**" .

Imetolewa na;

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Jubair" or "Jubairi".

Revocatus Kassimba

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.**